
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**

# MISINGI YA MAFANIKIO YA KITAALUMA KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA KUANZIA MWAKA 2013-2016




**OFISI YA MKURUGENZI,**
S.L.P 216,
**MPANDA -KATAVI.**
Simu: 025 – -252957128
Fax: NA 025-252957129
Baruapepe: **md@mpandamc.go.tz**

**JANUARI, 2017**

## DIBAJI

Halmashauri ya manispaa ya Mpanda ni miongoni wa Halmashauri tano katika Mkoa wa Katavi. Halmashauri ina jukumu la kutoa na kuinua ubora elimu kwa watoto na jamii. Ili kufanikisha azma hii, Halmashauri inazingatia mambo mbalimbali katika kuhakikisha inafikia malengo inayojiwekea kila mwaka kuanzia mwaka 2013 hadi 2016 .Ili kupata mafanikio inayolenga ,Halmashauri kuwashirikisha wadau wa Elimu wote yaani wazazi,walezi,walimu,viongonzi wa serikali ngazi zote,viongozi wa dini, viongozi wa kisiasa, na mashirika binafsi ili kuleta mabadaliko ya fikra chanya katika Elimu. Hivyo, tunaamini misingi ya mafanikio haya yakiendelea kutekelezwa kikamilifu itaendelea kuleta mafanikio katika Elimu Msingi kwa kuwaongezea hamasa na chachu wadau wetu wa Elimu kwa kuimarisha mifumo mbalimbali Mfano,Utoaji wa taarifa takwimu zinaanza na mwalimu,uteuzi wa viongozi,usimamizi wa kazi,kujiwekea malengo ya ufundishaji unaojenga maana,kuongea /kuwa karibu na wanafunzi watahiniwa na kuwaelimisha wadau wa elimu kuyatambua majukumu yao na kutimiza wajibu wao kikamilifu ili kuleta ufanisi wa elimu katika Halmashauri yetu.

## SHUKRANI

Mafanikio ya kufanya vizuri katika mitihani ya kumaliza Elimu Msingi katika Idara ya Elimu Msingi yametokana na kuongezeka kwa kiwango cha utendaji kazi cha walimu,kulikotokana kuongezeka kwa morali ya kufanya kazi,kuimarika kwa usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji kazi,mabadiliko na maboresho ya mifumo ya utendaji kazi pamoja ,ushirikishwaji kikamilifu wa wazazi katika kuimiliki Elimu ya watoto wao.Kwenye kila darasa na kuwa na mkakati iliyowekwa malengo ya kufikiwa kila mwaka. Mikakati hiyo imeasisiwa, kuboreshwa na kuendelezwa na wadau mbalimbali wa elimu, viongozi, kamati za shule na wataalam wote wa idara ya elimu Msingi toka ngazi ya shule, kata, vituo vya walimu (Klasta) na hamashauri ya manispaa ya Mpanda.

Kwahali hii tunawashukuru wale wote waliofanikisha uanzishwaji wa mipango Mikakati toka mwaka 2014 na hatimaye kufanikisha kwa kufaulisha zaidi kwenye mitihani mbalmbali hususani mitihani ya ya kumaliza elimu ya msingi toka mwaka 2014 ambapo Halmashauri imeshika nafasi ya kwanza kitaifa kwa miaka mitatu kwa mfululizohadi mwaka 2016.

Pamoja na shukrani kuwafikia wote, kwa umuhimu wao wafuatao wanatajwa kwa majina:Mh.Paza Mwamlima aliyekuwa Mkuu wa Wilaya (2012-2016),Mh.Enock Gwambasa aliyekuwa Menyekiti wa halmashauriya Mji na Aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa ndugu Suleiman Lukanga. Kwa sasa Mh.Lilian Matinga Mkuu wa Wilaya,Mh.William Mbogo Mstahiki Meya Manispaa ya Mpanda, Mwl Michael Nzyungu Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda, Leonard Simbeye Mhibiti Mkuu wa Ubora wa shule, Rehema Kilebwa Katibu wa TSD ,Maafisa Elimu Msingi,Maafisa Elimu Kata,na walimu wote .

Tunawashukuru sana wote kwa ubunifu na jitihada zao.

**Vicent B Kayombo**
**AFISA ELIMU MSINGI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA**
**MPANDA**

UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ina jumla ya tarafa 2, kata 15, mitaa 43, vijiji 14 na vitongoji 78.Ina jumla ya ukubwa wa eneo kilometa za mraba 527. Kutokana na sensa ya mwaka 2012 Halmashauri ina jumla ya wakazi 121,171, miongoni mwao wanaume 59,578 na wanawake 61,593.

Halmashauri ina jumla ya madarasa ya awali 36, miongoni mwa shule hizo shule 2 ni za watu binafsi na 34 ni za serikali, Pia ina shule za msingi 36, 34 zinamilikiwa na serikali na 2 watu binafsi pia kuna shule shikizi 3 ambazo zinamilikiwa na serikali.

Kwa mujibu wa TSM na TSA mwezi machi 2017 Halmashauri ya Manispaa ina jumla walimu 598, wanaume 258 na wanawake 340. Ina jumla ya wanafunzi 37,017 kati yao Wavulana 18,241 na wasichana 18,776.

Maendeleo katika idara ya Elimu ya msingi yamekuwa yakiongezeka tangu mwaka 2014, ufaulu umekuwa ukipanda kila mwaka ambapo kumekuwa na ongezeko la ufaulu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) kutoka asilimia 89.74 mwaka 2014 hadi asilimia 96.5 mwaka 2016. Ufaulu huo umeiwezesha Halmashauri ya manispaa ya Mpanda kushika **nafasi ya kwanza (1) kitaifa** katika halmashauri **zote** Tanzania Bara kwa **miaka mitatu (3) mfululizo.**

Mafanikio ya Kielimu katika Idara ya elimu msingi yamekuwa yakiongozwa na **DIRA** na **DHIMA** ya halmashauri pamoja na Uongozi thabiti wa elimu.

## 1.1 DIRA (VISION)

Halmashauri ya manispaa ya Mpanda inakusudia kutoa huduma bora za kiuchumi na kijamii kwa maendeleo endelevu.

## 1.2 DHIMA (MISSION)

Halmashauri ya manispaa ya Mpanda inasimamia na kulinda amani, kanuni na utoaji huduma bora za kijamii kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali kwa misingi ya utawala bora na kuondoa umaskini kwa ajili ya maendeleo endelevu.

## 1.4 TAFSIRI YA DIRA NA DHIMA YA ELIMU KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA

Kwa kuzingatia dira na dhima tajwa hapo juu, kielimu Halmashauri ya manispaa ya Mpanda inayo azma ya kuwa miongoni mwa Halmashauri bora zaidi kielimu kwa kuhakikisha inatoa Elimu bora kwa wanafunzi na jamii bila ubaguzi.

## 2.0 MATOKEO YA MITIHANI YA KITAIFA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA, 2013 HADI 2016

**Jedwali na. 1: Matokeo ya mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE), 2013-2016**

| MIAKA | 2013 | 2014 | ONGEZEKO | 2015 | ONGEZEKO | 2016 | ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| UFAULU KWA % | 62.87 | 89.79 | 26.92 | 97.89 | Hakuna | 96.5 | Hakuna |

Jedwali na. 1 linaonesha kuwa tangu mwaka 2013 Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ufaulu umekuwa ukipanda mfululizo,matokeo haya ni kama ifuatavyo;

- Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda imekuwa ya **Kwanza** kitaifa mfululizo kwa mwaka 2014,2015 na 2016.
- Kwa miaka 3 mfululizo Halmashauri ya Manispaa Mpanda imefikia **Lengo la Matokeo Makubwa sasa** (BRN) kama tulivyowekewa kitaifa.

## 3.0NGUZO ZA UTENDAJI KAZI

Nguzo za utendaji kazi zimegawanyika katika maeneo mawili ambayo Idara ya Elimu Msingi inaamini yakiwepo mafaniko katika Elimu yatafikiwa.Maeneo hayo ni ***Moyo wa kujituma kazini na Mfumo madhubuti wa usimamizi,ufatiliaji wa utendaji kazi na Tathimini***

### 3.1 MOYO WA KUJITUMA KAZINI

Idara Elimu Msingi imewajengea walimu wote na viongozi wanaosimamia ufundishaji na ujifunzaji kuwa na moyo wa kujituma na kujitolea katika utendaji wa kazi kwa maslahi mapana ya Halmashauri yao na Taifa kwa ujumla.Halmashauri inaamini kuwa Moyo wa kujituma kazini ni matunda ya uadilifu na nidhamu kwa walimu wake.

Kila kiongozi wa idara ya elimu manispaa ya Mpanda anapaswa kuwa na moyo wa uzalendo kwa kufanya kazi kwa bidii kwa kuzingatia ***matokeo*** (Perfomance For Results) ambao huleta mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 3.2 MFUMO MADHUBUTI WA USIMAMIZI,UFATILIAJI WA UTENDAJI KAZI NA TATHIMINI

Mafanikio ya idara ya elimu msingi yanategemea sana mfumo madhubuti wa usimamizi ,ufuatiliaji wa utendaji kazi na Tathimini.Katika kusimamia utelezaji

wa mifumo ya usimamizi, ufuatiliaji na Tathimini Idara imefanya mabadiliko makubwa ya kifikra kutoka kwenye utendaji wa mazoea kwenda kwenye utendaji usio wa mazoea ,unaozingatia **matokeo** na unaofuata taratibu ,kanuni na sheria. Idara imesimamia ufundishaji unaozingatia ujenzi wa maana na unaomfanya mwalimu ajitathimini sababu za uwepo wake kwenye eneo husika.Ili kufanikisha malengo yanayowekwa, viongozi mbalimbali wanashirikishwa katika Usimamizi,ufuatiliaji na Tathimini, viongozi hao ni :- Mkuu wa Wilaya, Mstahiki meya, Waheshimiwa Madiwani, Mkurugenzi wa Manispaa, Viongozi wa elimu na idara zote za Manispaa kwa ngazi ya wilaya na Halmashauri. Maafisa tarafa, Waratibu wa vituo vya Walimu, Watendaji wa Kata, Maafisa Elimu kata, Wenyeviti wa Mitaa/vijiji, maafisa watendaji Mitaa/vijiji, Kamati za shule, walimu wakuu, walimu wote, wadau wa elimu na wanafunzi wenyewe.

## 4.0 MISINGI YA MAFANIKIO

- Yapo mambo kadhaa yanayosaidia Halmashauri kufanya vizuri kitaaluma kimkoa na kitaifa kwa mara ya tatu mfululizo kuanzia mwaka 2013 hadi 2016.Mambo hayo yapo katika misingi kumi na mbili(12).

Misingi hiyo ni :-

### 4.1 **UWEPO WA MIPANGO INAYOWEKA KAZI ZA KUFANYA NA MATARAJIO KWA KILA KAZI NA KILA MDAU**

Idara ya elimu Msingi katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda hufanya kazi kwa kuweka Malengo ya kufika kwa kila mwaka kupitia Mpango wa muda mfupi (**short term**) na Mpango wa muda mrefu( **Long term plan**). Kwa kupitia Mpango wa muda mfupi,Idara huweka Mpango Mkakati wa kila Mwaka, Mwaka 2017 Idara itafanya kazi kwa kutumia Mpango Mkakati wa Magamba ( **The Magamba Strategic Plan -2017).** Uwepo wa Mipango umesaidia wadau wote kufanya kazi kwa nia ya kufikia lengo moja.

### 4.2 KUIMARISHA UONGOZI NGAZI YA SHULE,KATA,NA VITUO VYA WALIMU (KLASTA)

I. Idara imeweka utaratibu wa kuandaa walimu kuwa viongozi kwenye ngazi mbalimbali (Succession Planning) .Mfano,walimu wakuu wasaidizi huteuliwa kuwa walimu wakuu na walimu wakuu huteuliwa

kuwa Maafisa Elimu Kata na vituo vya walimu.Utaratibu huu huongeza uwajibikaji kwa viongozi

II. Uteuzi wa walimu wakuu wasaidizi ufanya na Afisa Elimu wa Manispaa ;utaratibu huu umejenga nidhamu na heshima kwa msaidizi wa Mwalimu Mkuu

**N:B :** Uteuzi wa viongozi huzingatia uwezo wake kiutendaji,uadilifu,moyo wa kujituma katika kazi na kiwango chake cha Elimu

### 4.3 KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU

Utoaji wa huduma bora kwa walimu ni mojawapo ya nyenzo muhimu ya Halmashauri kupiga hatua kitaaluma mwaka hadi mwaka.

I. Kuwatembelea Walimu Vituoni (outreach)
II. Stahiki za walimu

III. upandishaji wa madaraja kwa walimu

### 4.5 Mfumo madhubuti wa usimamizi,ufuatiliaji wa utendaji wa kazi na Tathiminiss

I : Ufuatiliaji wa Afisa Elimu Mlezi na Afisa Elimu wa Kata
II: Ufuatiliaji wa jopo
III:Ufuatiliaji wa Mkurugezi wa Manispaa
IV: Ufuatiliaji kwa njia ya fomu

### 4.6 USHIRIKIANO KATI YA IDARA YA ELIMU MSINGI NA OFISI YA MTHIBITI UBORA WA SHULE

Idara ya uthibithi ubora wa shule hufanya kazi begakwa began a Idara ya elimu Msingi.Mkaguzi wa shule hukagua shule na kutoa taarifa ya ukaguzi kwa Mkurugenzi ambaye kupitia Idara ya Elimu Msingi hutekeleza maelekezo na ushauri unaotolewa na wathibiti wa ubora wa shule.

### 4.7 UWEPO WA MIKUTANO MBALIMBALI

I: MIKUTANO YA WALIMU
II MIKURANO YA WAZAZI
III MIKUTANO YA KAMATI YA SHULE
IV MIKUTANO YA WATENDAJI WA KATA NA MITAA
V Mikutano ya kazi

### 4.8 UKAMILISHAJI WA MADA ZOTE KWA WAKATI.

(i). Darasa la saba
(ii). Darasa la nne
(iii). Madarasa mengine

**4.9 UTOAJI WA MOTISHA KWA WALIMU**

Halmashauri imeweka utaratibu wa kutoa motisha kwa walimu, wanafunzi na kamati za shule kila wanapofanya vizuri kitaaluma na Nyanja nyingine. Zawadi za vyeti na fedha taslimu hutolewa kwa makundi yanayofanya vizuri kila mwaka.

**4.10HAMASA KUTOKA VIONGOZI MBALIMBALI**

Idara ya Elimu Msingi imekuwa ikipata uungwaji mkono kutoka kwa viongozi mbalimbali katika kutekeleza mikakati yake hususani Mkuu wa Wilaya, na Mkurunzi wa Halmashauri wamekuwa wakitoa ushirikiano wa hali na mali katika kutekeleza malengo ya idara. Mfano kutoa fedha za kuendeshea mitihani ya majaribio pamoja na kuwahudumia walimu kwa wakati.

**4.11MAFUNZO KAZINI**

Halmashauri inaratibu na kusimamia uendeshaji wa mafunzo kazini kwa walimu. Mafunzo haya yamegawanyika katika makundi mbalimbali.

(i). Semina na mafunzo ya mada ngumu.
(ii). Mafunzo ya kuongeza ujuzi
(iii). Mafunzo ya uongozi kwa walimu wakuu.
(iv). Mafunzo ya matumizi ya fedha na manunuzi.
(v). Mafunzo ya muda mrefu

**4.12UWEPO WA MASOMO REKEBISHI KWA SHULE ZA MSINGI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO 2013-2017.**

Mpango huu uliibuliwa na wataalamu wa Elimu wa Idara ya Elimu Msingi waliokutana huko sekondari ya Milala Mpanda kutathimini ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kuongeza kiwango cha ufaulu na namna ya kutatua changamoto mbalimbali.Changamoto hizo ni pamoja na:-

i. Uhaba wa walimu
ii. Uhaba wa miundombinu ya shule –
iii. Ukosefu wa madarasa ya Elimu ya Awali katika baadhi ya shule
iv. Maelekezo mbalimbali ya serikali kuu
v. Kuyaandaa madarasa ya mitihani

Mpango wa Masomo Rekebishi una aina mbalimbali za masomo yanayotolewa kutegemeana na muda na aina ya wanafunzi kama ifuatavyo:-

1) Saa 1:00 hadi 2:00 asubuhi Jumatatu hadi Ijumaa.
**2)** Saa 9:30 hadi 12:30 jioni Jumatatu hadi Ijumaa**.**

3) Saa 2:00 asubuhi hadi saa 7:00 mchana Jumamosi na siku za sikukuu.

**HITIMISHO**

Kupanda kwa taaluma katika Halmashauri ya Manispaa Mpanda kumetokana na uzingatiaji wa mambo yaliyoelezwa hapo juu pamoja na mambo mengine mengi ambayo yamekuwa yakibadilika kulingana na wakati na matukio mbalimbali.

Ni imani ya Idara na halmashauri kwa ujumla kuwa uzingatiaji wa misingi 12 iliyofafanuliwa hapo juu pamoja na misingi mingine kutegemeana na mazingira unaweza kuinua ufaulu katika eneo lolote ndani ya Tanzania endapo viongozi katika eneo husika watakuwa na dhamira ya dhati ya kuinua taaluma katika eneo wanaloliongoza.